



Tanzania Human Rights Defenders Coalition [THRD-Coalition]

P. O. Box 105926 Dar es Salaam, TANZANIA Mob: +255 783 172394 E-mail:
defenderscoalition@rocketmail.com, web www.thrdc.or.tz

TAMKO KWA VYOMBO VYA HABARI DHIDI YA KUVAMIWA NA KUUWA KWA ASKARI WA JESHI LA POLISI

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania ni mwamvuli wa mashirika zaidi ya 100 yanayotetea Haki za Binadamu hapa Tanzania. Mashirika haya kwa pamoja tumepokea taarifa za kusikitisha za majambazi kuvamia kizuizi cha polisi barabara ya Kilwa mpakani mwa Mkurunga na Dar es Salaam na kuua askari polisi wawili na kujeruhi mmoja na kisha kupora bunduki mbili aina ya SMG.

Tukio hilo limeshathibitishwa na kulaaniwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mathias Chikawe na Tume ya Utawala bora na Haki za Binadamu. Askari waliouawa ni D.2865 SGT Francis na E.177 CPL Michale wakati aliyeruhiwa ni D 5573 SGT Ally.

Mtandao unapenda kutoa pole kwa Jeshi la Polisi na ndugu za marehemu na watanzania kwa ujumla kwa kupoteza nguvu kazi ya taifa, na kulaani vikali matukio ya mauaji kwa jeshi la polisi na uvamizi kwani kwetu sisi kama mtandao tunawaona Polisi wote ni watetezi wa Haki za Binadamu.

Hali ya Sasa ya Usalama

Kumekuwa na hali tete ya usalama hasa kwa Jeshi la Polisi kwa mwaka 2015. Mfano kwa mwaka huu 2015 Mtandao umerekodi matukio zaidi ya 4 ya uvamizi na mauaji ya Polisi, mfano mwanzoni mwa mwaka 2015 kulifanyika uvamizi Ikwiriri na polisi wawili wakupoteza maisha, tarehe 2 febuari 2015 kulifanyika uvamizikatika kituo cha Polisi Mgeta Kilombero Morogoro na majambazi kuchukua silaha za kivita SMG, Tukio lingine lilitokea tarehe 4 mwezi wa pili mwaka 2015, Polisi mmoja G. 716 PC alipoteza maisha akijaribu kumlinda mtoto aliyekuwa akipigwan na mzazi wake.

Matukio yote haya ya uvamizi na mauaji ya kwa Jeshi la Polisi ni ya kulaani na kukemewa na wadau wote, hasa katika kipindi hichi cha kuelekea katika uchaguzi.

Wito wetu

a) Kwa Umma

- Tunaomba jamii kushirikiana na Jeshi la Polisi kuwatambua wahusika waliohusika na uvamizi na mauaji katika tukio hili la Kilwa . Jamii ikumbuke kwamba Polisi ni ndugu zetu sote, hivyo basi tuchukue jukumu kama jamii kuwalinda kama wanavotulinda.
- Kuwatambua Polisi kama watetezi wa Haki za Binadamu kwa kuwa hulinda maisha yao na mali zao.

b) Kwa Jeshi la Polisi

- Tunaliomba Jeshi la Polisi kuacha kupokea amri ambazo ni kinyume na utendaji wao wa kazi, hii italeta mahusiano mazuri kati ya jamii na polisi
- Hasa katika kipindi hiki tunachoelekea katika uchaguzi, tunaliomba Jeshi la Polisi kuzidisha ulinzi na usalama katika vituo vyote vya Polisi na kwa raia.
- Jeshi la polisi linapaswa kutambua njia mpya na rafiki za kupambana na makosa kama Ugaidi, Makosa ya mitandao ya kijamii na usafirishaji haramu wa binadamu.

c) Kwa watendaji wa Serikali na vyama vya siasa

Kuacha kulitumia Jeshi la Polisi kuwapa amri ambazo zitapelekea ukiukwaji wa haki za binadamu, na kuwatumia polisi kutimiza maslai yao binafsi, kwakuwa mwisho wa siku chuki inayojengeka katika jamii inawaathiri Polisi na sio watoa amri.

Imetolewa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania kwa niaba ya wanachama,



**ONESMO OLENGURUNWA
MRATIBU KITAIFA**